# Majukumu ya Wabunge katika kutokomeza ndoa za utotoni:

## Na “Watoto wa kike si Mabibi Harusi”



GIRLS NOT BRIDES | The Global Partnership to End Child Marriage

# Utangulizi

Mtoto wa kike anapokuwa bibi harusi matokeo yake ambayo siyo mazuri ni katika maisha yake yote, kwa watoto wake na kwa taifa. Kila mwaka wasichana 15 millioni duniani wanaolewa wakiwa watoto.
Zaidi ya wanawake milioni 720 walio hai leo waliolewa au waliingia katika mahusiano kabla ya kufikia miaka 18. Ndoa za utotoni zinafanyika katika nchi mbali mbali, tamaduni, dini na makabila.
Kama hakutakuwepo na hatua za kupunguza ndoa hizo katika miaka ya karibuni, wasichana billioni 1.2 watakuwa wameolewa wakiwa watoto ifikapo mwaka 2050.

Sababu ya msingi ya ndoa za utotoni ni kutokuwepo usawa wa kijinsia na thamani ya chini wanayopewa wasichana. Hali hiyo inaongezeka kutokana na umaskini, kukosekana usalama na kuwepo migogoro. Ndoa hizo zinawanyima wasichana haki zao na kudhoofisha vipaumbele mbali mbali vya maendeleo. Kukomesha ndoa za utotoni kutahitaji hatua endelevu za muda mrefu katika sekta kadhaa. Mfumo imara wa sera na sheria kwa ajili ya kuzuia ndoa za utotoni na kuwalinda watoto walioolewa ni msingi katika hatua za serikali za kuzishughulikia taratibu hizo.

Wabunge wako katika nafasi ya kipekee ya kuweza kubuni, kuendeleza na kutekeleza mfumo katika nchi na nje ya mipaka yake. Wabunge wanaweza kutoa mwongozo katika kutekeleza sheria na sera zinazotakiwa, kupitisha bajeti, kufuatilia utekelezaji na kuhakikisha uwajibikaji kulingana na ilivyodhamiriwa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Wabunge wanaweza kuhakikisha kwamba sauti za wananchi zinasikika ikiwa ni pamoja na zile za watoto wa kike, ili kuweza kuhamasisha utashi na dhamira ya kisiasa ya kukomesha ndoa za utotoni.

Hata hivyo, Wabunge mara nyingi hawatambuliki kama ni wadau muhimu na waletaji mabadiliko katika suala hili. Kijitabu hiki chenye maelekezo kinalenga kutoa mifano thabiti na mapendekezo kuhusu namna Wabunge wenye nia watakavyoweza kuchukua hatua. Zaidi ya hayo, kijitabu hiki kinakuza mahusiano na asasi za kiraia zinazoshughulikia suala hili la ndoa za utotoni.

Ni mategemeo yetu kijitabu hiki kitatoa hamasa ya kuungana na harakati za kimataifa kuhusu kutokomeza ndoa za utotoni na kuimarisha juhudi zenu kama Wabunge. Tunaamini kwamba, kwa kuanzisha mahusiano ya muda mrefu na Wabunge wenye dhamira njema tunaweza kufanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya dunia ambapo wasichana na wanawake wanafurahia haki sawa pamoja na wavulana na wanaume.

Tunawatakia mafanikio ya kila namna katika jitihada zenu za kutokomeza ndoa za utototni na kufanikiwa kutambua haki za kila msichana.

**Heather B. Hamilton**
Mshauri Mwandamizi na Mratibu wa Mpito wa Kimataifa
*“Watoto wa Kike si Mabibi Harusi”:* Ushirikiano wa Kimataifa wa Kutokomeza Ndoa za Utotoni

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| **1. Madhumuni** | 4 |
| **2. Kuhusu Ndoa za Utotoni: maana na zilivyoenea ulimwenguni** | 5 |
| **3. Wahusika na athari za ndoa za utotoni** | 7 |
| **4. Sheria na Ndoa za Utotoni** | 9 |
| **5. Jukumu la Wabunge katika kutokomeza ndoa za utotoni** | 12 |
| **6. Wabunge wanaweza kufanya nini?** | 13 |
| **7. Viambatisho** | 15 |
| i. Makala kutoka katika Mikataba ya Kisheria ya Kimataifa kuhusu ndoa za utotoni | 15 |
| ii. Sampuli ya Maswali ya kuwauliza wenye mamlaka ya kufanya maamuzi | 17 |
| iii. Sampuli ya ujumbe kwa ajili ya mitandao ya kijamii | 18 |
| iv. Taarifa za kuchukua kutoka kwenye mitandao | 19 |
| v. Machapisho kuhusu ndoa za utotoni na Sheria | 20 |
| vi. Taarifa za kijumla na takwimu | 20 |
| vii. Vifupisho | 20 |
| viii. Maelezo ya mwisho | 21 |

# 1 Madhumuni

**Serekali ulimwenguni zina dhamira ya kumlinda mtoto wa kike. Asasi iitwayo *"Watoto wa kike si Mabibi Harusi"* imetambua mikakati mathubuti ya kisheria na kisera kama mfumo mmoja wapo kati ya minne ikiwa ni pamoja na wanachama wake zaidi ya 430 duniani kote kwa ajili ya kutokomeza taratibu potofu kuhusu ndoa za utotoni**[1].

Mara nyingi lengo la kutokomeza ndoa za utotoni ni kuhakikisha umri wa chini wa kuolewa uwe miaka 18, hata hivyo mpangilio mpana wa sheria na sera vinahitajika kuwepo ili kuwalinda wasichana walio katika hali hatarishi na kuwalinda wasichana wadogo walioolewa ili kuhakikisha wanafikia uwezo wao. Wabunge ni wadau muhimu katika kutokomeza mimba za utotoni, kwa sababu wanaweza wakawa mstari wa mbele katika kutunga sheria na sera husika, kupanga rasilimali kutoka kwenye bajeti za kitaifa, kufuatilia utekelezaji na kuhakikisha, kuwepo kwa uwajibikaji.

Kijitabu hiki kina lengo la kuwapatia Wabunge taarifa ya jumla kuhusu ndoa za utotoni zina maana gani ikiwa ni pamoja, na wahusika muhimu, kuenea kwake ulimwenguni na matokeo yake. Lengo maalum linaelekezwa kwenye vyombo vya sheria vilivyopo mbavyo vinakataza tamaduni potofu ikiwa linajumuisha pia mapendekezo thabit kwa ajili ya Wabunge ili waweze kuchukua hatua siyo tu ndani ya Bunge bali pia katika majimbo yao na ngazi ya kimataifa.

Watoto wa Kike si Mabibi Harusi:

### Ushirikiano wa Kimataifa wa Kutokomeza Ndoto za Utotoni

*"Watoto wa Kike si Mabibi Harusi":*
ni ushirikiano wa kimataifa wa asasi za kiraiza ya zaidi ya 400 zinazoshughulikia ndoa za utotoni. *"Watoto wa Kike si Mabibi Harusi" wameunganishwa na dhamira* ya kutokomeza ndoa za utotoni na kuwawezesha wasichana kufikia uwezo wao.

Kwa pamoja wanachama wanafanya kazi ya kutokomeza ndoa za utotoni ifike katika ufahamu wa kiulimwengu na uelewa wa nini kinatakiwa.

*"Watoto wa kike si Mabibi Harusi"* wanatoa rai kwamba sheria, sera na programu ziwepo kwa ajili ya kubadilisha maisha ya mamilioni ya wasichana.

Utapata zaidi kutoka: www.GirlsNotBrides.org au wasiliana na: info@GirlsNotBrides.org

# 2 Kuhusu Ndoa za Utotoni: Maana na jinsi zilivyoenea ulimwenguni

## *Ufafanuzi*

***“Ndoa ya Utotoni”*** ni ndoa rasmi au muungano usiyo rasmi ambapo mmoja wa wanandoa ni mtoto. Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto unafafanua kuwa: “mtoto ni binadamu yoyote ambaye kiumri yuko chini ya miaka kumi na nane isipokuwa pale ambapo sheria imetamka vinginevyo.” Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto imetoa rai kwa Serikali wanachama kurejea sheria ili umri wa mtoto usizidi miaka 18.

***Ndoa za ‘mapema”*** mara nyingi inatumika pamoja na neno **“ndoa za utotoni”** na ina maana ya ndoa inayomhusisha mtu chini ya miaka 18 katika nchi ambapo umri wa mtu mzima unafikiwa mapema au kutokana na ndoa. Ndoa ya mapema inafafanuliwa kuwa wanandoa wana umri wa miaka 18 au zaidi lakini kuna mambo yanayowafanya wasiwe tayari kuamua kuoana kwa mfano kiwango cha kukua kimaumbile, kihisia, kingono, kisaikolojia au kukosekana taarifa kuhusiana na chaguzi za maisha binafsi.[2]

***‘Ndoa ya lazima”*** ni ndoa yoyote inayotokea bila ridhaa huru na kamili ya mmojawapo wa wanandoa au wote na/au pale ambapo mmoja wapo au wote hawana uwezo wa kuacha au kujitoa kwenye ndoa ikiwa ni pamoja na kutokana na shinikizo kubwa la kijamii na kifamilia.

## Ndoa ya utototoni: Utaratibu wa jadi wenye madhara

Kila kikundi cha kijamii duniani kina mila na desturi zake mahususi, baadhi ya mila hizo zina manufaa kwa wanajamii wote wakati nyingine zina madhara, kwa baadhi ya vikundi. Ndoa za utototni, ukeketaji na mifumo ya ulipaji wa mahari,ni baadhi ya mifano ya mila na taratibu potofu. Mila zinazoathiri wanawake na watoto wa kike zina maumivu ya kimwili, na madhara kiakili ya muda mrefu na mfupi kwa waathirika na zina madhara makubwa katika maendeleo ya mtoto wa kike.

Katika tamko la pamoja, taasisi za Umoja wa Mataifa zilibainsha kuwa “[…] haikubaliki kuwa jamii ya kimataifa inabakia kama mtazamaji tu kutokana kutokueleweka kwa maono juu ya kuingiliana kwa tamaduni, tabia za binadamu, tunu za kitamaduni, hata pale zinapoonekana za kipuuzi au ni haribifu kutokana na mtezamo wa mtu au utamaduni mwingine lakini bado zina maana na kazi kwa wale wanaotumia mila na taratibu hizo. Utamaduni haugandi, unajirekebisha na kuleta mageuzi. Watu watabadilisha tabia wakielewa madhara ya mila potofu zinazoathiri utu wa mtu na pia inawezekana kuachana na mila potofu bila ya kuacha vipengele vya tamaduni zenye maana”.

*(WHO, Female Genital Mutilation: A Joint WHO/UNICEF/UNFPA Statement. 1996)*

## *Kiwango: Ndoa za Utotoni ni tatizo la kimataifa*

- Takriban wasichana million 15 wanaolewa kila mwaka kabla hawajafikia miaka 18. Hii [3] ni kama watoto wa kike 41,000 kila siku.
- Ndoa za utotoni hutokea duniani kote, na kila nchi, tamaduni, dini na makabila:
  45% ya watoto wa kike chini ya miaka 18 wameolewa Asia ya kusini; 41% Afrika chini ya Janjwa la Sahara; 29% America ya Kusini na Caribbean; 18% Mashariki ya Kati na Afrika ya Kaskazini; na zinatokea pia katika baadhi ya jamii huko Ulaya na Amerika ya Kaskazini[4].
- Katika dunia inayoendelea, 1 kati ya watoto wa kike 3 wanakuwa wameshaolewa wafikapo miaka 18, na 1 kati ya 9 anakuwa ameolewa afikapo 15 na wengine 8 au 9[5].
- Wakati kumekuwepo na mwelekeo chanya katika baadhi ya nchi, ndoa za utotoni katika ngazi ya kimataifa hazijabadilika katika muongo uliopita.
  Hata hivyo[6], tofauti kubwa katika mabadiliko katika viwango vya ndoa za utotoni vinaonekana katika baadhi ya kanda na nchi.

### Ndoa za Utotoni Zilivyoenea Katika Nchi Mbalimbali*

| | |
|---|---|
| 70%+ | Niger. |
| 69-60% | Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Bangladesh. |
| 59-50% | Mali, Guinea, Burkina Faso, Sudan ya Kusini, Malawi. |
| 49-45% | Mozambique, India, Somalia. |
| 44-40% | Sierra Leone, Zambia, Nigeria, Madagascar, Ethiopia, Jamhuri ya Dominica, Nepal, Nicaragua, Eritrea, Afghanistan, Cuba, Uganda. |
| 39-35% | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Cameroon, Liberia, Tanzania, Gambia, Brazil, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao. |
| 34-30% | Benin, Sao Tome na Principe, Mauritania, Honduras, Congo, Côte d'Ivoire, Senegal, Sudan, Yemen, Zimbabwe, Guatemala, Comoros, Equatorial Guinea. |
| 29-25% | Nauru, Kenya, Visiwa vya Marshall, Belize, Bhutan, El Salvador, Togo. |
| 24-20% | Iraq, Pakistan, Colombia, Guyana, Mexico, Visiwa vya Solomon, Ecuador, Guinea-Bissau, Gabon, Bolivia, Papua New Guinea, Ghana, Taifa la Palestina, Burundi, Kiribati, Thailand, Costa Rica. |

* Asilimia ya wanawake wenye umri 20-24 ambao waliolewa au katika mahusiano kabla ya kufikia miaka 18 *(UNICEF State of the World's Children, 2014)*.

# 3 Wahusika wa kuchukua hatua na athari za ndoa za utotoni

## *Wahusika wa kuchukua hatua*

**Mambo ambayo kusababisha ndoa za utotoni ni; umaskini, wasiwasi kuhusu usalama na ulinzi wa wasichana, kukosa elimu au umbali wa kufika shuleni, ubaguzi wa kijinsia; mila na tamaduni, na taratibu za dini.**

- **Tamaduni:**: Ndoa za utotoni ni taratibu za jadi. Na katika sehemu nyingi zinaendelea kwa sababu tu zimekuwepo vizazi na vizazi – na kutokufuata mila kunaweza kusababisha mtu kutengwa na jamii.
- **Majukumu ya Kijinsia**:: Katika jamii ambapo kuna ndoa za utotoni, wasichana hawapewi thamani kama ilivyo kwa wavulana – wao huonekana kama mzigo. Changamoto itakuwa kubadilisha mtazamo wa wazazi na kuweka msisitizo kwamba wasichana watakaoepuka ndoa za mapema na kubaki shuleni kuna uwezekano wa wao kutoa michango kwenye familia na jamii zao katika siku za mbeleni.
- **Umaskini:** Pale ambapo umaskini umekithiri, kumtoa mtoto wa kike akaolewe inatoa fursa kwa wazazi kupunguza gharama za kutunza familia kwa kupunguza mtu mmoja wa kulisha, kumvisha na kumwelimisha. Mahari inayolipwa ni pato linalotegemewa katika familia maskini. Kule ambako familia inalipa mahari kwa ajili ya bwana harusi mara nyingi malipo ni kidogo kama bwana harusi ni mdogo kiumri na hana elimu.
- **Usalama**: Wazazi wengi wanawaozesha wasichana wao wadogo kwa kudhani ni kwa ajili ya maslahi yao, mara nyingi kwa ajili ya usalama wao katika maeneo yenye hatari ya kushambuliwa kimwili na kingono.
- **Sheria:** Kuna kukosekana mfumo wa kisheria wa kutosheleza kushughulikia kesi za mimba za utotoni. Wakati katika nchi nyingi sheria zimeweka umri wa chini wa kuolewa au kuoa lakini mara nyingi sheria hizo, hazitekelezwi inavyotakiwa.
  - Mfumo dhaifu wa kuandikisha vizazi ina maana inazuia wasichana kutoa uthibitisho kwamba ni wadogo kwa ajili ya ndoa. Ukiondoa Uchina, watoto walioandikishwa baada ya kuzaliwa katika nchi zinazoendelea ni 51% tu katika kipindi cha 2000 – 2009.[7]
  - Ukosefu wa kuoanisha sheria za kimila ambazo zingeweza kushughulikia taratibu za ndoa za utotoni. Ndoa za utotoni ziko zaidi katika maeneo ambako mamlaka zinatoa nafasi finyu za kuwalinda wanawake na watoto.

## *Athari: kwa nini ni muhimu kujadili ndani ya Bunge?*

Athari za mimba za utotoni katika kuhakikisha watoto na wanawake wanafurahia haki zao za kibinadamu zinaweza kuwa pana, ikiwa ni pamoja na kuhusiana na umaskini, elimu, kutokuwepo usawa wa kijinsia, afya, nakadhalika.

## *Ndoa za utotoni zina uhusiano na umaskini na zina athari kwenye tija kitaifa*

- Ndoa za utotoni ziko zaidi katika nchi ambazo ni maskini duniani na mara nyingi zinaongezeka katika kaya maskini zaidi. Zinahusiana zaidi na ngazi za chini za maendeleo ya kiuchumi.
- Uwezekano wa watoto wa kike kuolewa kabla ya miaka 18 ni mara mbili kwa kulinganisha na wenzao, kutoka familia tajiri kwa sababu ndoa zinaonekana kama namna ya kumpa msichana maisha ya baadaye.[8] Hata hivyo, wasichana hao wana uwezekano wa kuwa maskini na kubakia maskini.[9]
- Wasichana wanaoolewa wakiwa wadogo hawapati fursa za elimu na za kiuchumi ambazo zinasaidia kuwatoa katika umaskini ambavyo ni muhimu kwa ajili ya kujenga mustakabali endelevu na wenye mafanikio kwa ajili ya jamii na taifa[10].
- Wanawake wenye afya na elimu wanaongeza mchango wao katika pato la taifa. Wanatumia fedha zao kwenye chakula, malazi, elimu na miradi ya kutengeneza kipato; vyote hivyo vinachangia kupunguza viwango vya umaskini na kukuza maendeleo endelevu.

## Ndoa za utotoni huathiri haki ya mtoto ya elimu

- Ndoa za utotoni zinawanyima watoto wanaotakiwa kuwa shuleni haki yao ya elimu ambayo wanaihitaji kwa ajili ya maendeleo binafsi, maandalizi ya kuwa watu wazima na uwezo wao wa kuchangia katika familia zao na jamii.
- Watoto wa kike walioolewa na wangependa kuendelea na shule kiuhalisia na kisheria wanaweza wakawa wamezuiliwa. [11] Ndoa mara nyingi ina maana mwisho wa elimu kwa wasichana.
- Msichana akibakia shuleni kwa muda mrefu, anapunguza uwezekano wa kuolewa akiwa chini ya miaka 18 na kuzaa watoto katika miaka yake ya utotoni.
- Zaidi ya 60% watoto mabibi harusi katika nchi zinazoendelea hawana elimu iliyo rasmi.
- Viwango vya juu vya elimu vinapunguza uwezekano wa ndoa za utotoni. Kuwaelimisha vijana ni muhimu katika ulimwengu ambapo nusu ya watu ni chini ya miaka 25 ili kuhakikisha mustakabali wa baadaye wenye mafanikio.

## Ndoa za totoni, vifo vya watoto wachanga afya ya uzazi

- Mabibi harusi watoto wanakuwa chini ya shinikizo kubwa la kijamii ili kuthibitisha uwezo wao wa kuzaa, ambayo ina maana inaongeza uwezekano wa kupata mimba mapema na za mara kwa mara.[14]
- Matatizo ya mimba na wakati wa kujifungua ndiyo chanzo cha vifo vya wasichana wenye umri wa miaka 15-19 katika nchi zenye uchumi wa chini na wa kati. 90% ya mimba za utotoni katika nchi zinazoendelea ni kwa watoto wa kike ambao tayari wako kwenye ndoa.[15]
- Wengi wa watoto mabibi harusi wanapata mimba kabla miili yao haijawa tayari kubeba mimba au kujifungua watoto; kitu kinachoathiri afya zao. Hali ni mbaya zaidi kwa wasichana wanaozaa kabla ya kufikia umri wa miaka 15 na uwezekano wa vifo ni mara tano zaidi kulinganisha na wenzao walio katika miaka yao ya 20.[16]
- Kiwango cha watoto wanaofia tumboni na wale wanaofariki katika wiki moja toka kuzaliwa ni 50% kwa wazazi chini ya miaka ishirini kulinganisha na wenzao wa miaka 20 - 29.[17].

## Ndoa za utotoni zinasisitiza kutokuwepo usawa wa kijinsia

- Watoto mabibi harusi hawana maamuzi kuhusu lini na ni nani awaoe. Mara nyingi waume zao wanakuwa wa umri mkubwa zaidi.
- Wasichana wanaoolewa kabla ya miaka 18 wana uwezekano wa kufanyiwa vitendo vya ukatili kuliko wenzao walioolewa baadaye[12].
- Ndoa mara nyingi ndiyo mwisho wa fursa ya elimu kwa wasichana, kupata kazi za mshahara nje ya nyumbani na uwezo wa kuwa wa majukumu ya kufanya maamuzi katika jamii. Kutokomeza kutokuwepo usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake vijana inahitaji kutimiza mahitaji muhimu na haki zao ikijumlisha elimu, afya na chakula bora ambavyo vinaathiriwa na ndoa za utotoni.[13]

## Ndoa za Utotoni na ukatili wa kingono na ukatili wa kijinsia

- Ndoa za utotoni zinawaweka wanawake na watoto wa kike katika hatari ya kufanyiwa ukatili wa kingono, kimwili na kisaikolojia katika maisha yao yote. Wasichana wanaoolewa wakiwa chini ya miaka 18 wanafanyiwa unyanyasaji wa majumbani kuliko wenzao wasioolewa na hawatoi taarifa kuhusu kubakwa mara ya kwanza wanapofanya tendo la ndoa.
- Katika maeneo ambayo wasichana wako katika hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia, wazazi wanachagua kuwaoza watoto wao wa kike kwa kuamini ndoa inahakikisha usalama wao. Wasiwasi huo ni wa kweli, lakini ndoa ya mapema haitoi usalama mbadala.
- Kama watoto, ni mara chache wakiwa mabibi harusi wanathubutu kudai matakwa yao kutoka kwa waume zao ambao ni watu wazima zaidi, kujadili kuhusu ngono salama na ya hiari. Wana uwezekano wa kuamini kuwa ni haki mwanamume ampige mke wake mara kadhaa kuliko wanawake wanaoolewa baadaye.

# 4 Ndoa za utotoni na sheria

**Ndoa za utotoni ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unaoathiri wanawake, na watoto na haki zao za elimu, usawa, kutokubaguliwa, na uhuru wa kuishi bila ubaguzi na unyonyaji. Hizi ni haki zilizoko katika Azimioa la Kimataifa juu ya Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (MKHM), Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya, Wanawake pamoja na mikataba mingine ya haki za binadamu ya kimataifa na kikanda.**

### *Kwa nini ni muhimu kwa nchi kuwa na umri wa chini wa kuolewa/kuoa kisheria?*

Sheria zinazoweka umri wa chini wa kuingia kwenye ndoa ni muhimu kwa ajili ya kuwalinda wasichana na wavulana wasiingie kwenye ndoa wakiwa siyo tayari kimaumbile, kiakili na kihisia. Kwa nini watoto waingizwe kwenye ndoa wakiwa na umri ambao hauwaruhusu kwa mfano, hawana haki ya kupiga kura au kuingia kwenye mkataba unaotambuliwa kisheria?

Ufafanuzi unaokubalika kwa wengi juu ya maana ya mtoto ni mtu yoyote chini ya miaka 18, kwa kulingana na Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto. Ni muhimu watoto watambuliwe kisheria kuwa ni watoto na wapewe ulinzi kamili.

Nchi tofauti zina mbinu mbambali za kisheria; nyingine zimepitisha ndoa za utotoni kuwa ni jinai; nyingine zimepiga marufuku au kubatilisha ndoa chini ya umri wa chini uliokubaliwa kisheria; na nyingine zimetoa agizo kuhusu umri wa chini wa ndoa bila kuwa wazi kuhusu kama ni kosa la jinai au kupiga marufuku.

Serikali zinatakiwa ziwe na sheria wazi na thabiti zinazotamka miaka 18 kama ni umri wa chini wa kuingia kwenye ndoa. Ulinzi wa kutosha unatakiwa uwepo ili kuhakikisha ruhusa ya wazazi na vizuizi vingine havitumiwi ili kulazimisha wasichana waolewe kwa nguvu.

## Mikataba ya kisheria ya Kikanda: Mfano wa Afrika

Afrika ina Mikataba ya Kisheria kwa mfano; Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na za Watu juu ya Haki za Wanawake Afrika na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto (MAHUM) ambayo ina tamko juu ya Ndoa za Utotoni. Katika Ibara ya 21 juu ya Kinga dhidi ya taratibu za mila na tamaduni zenye madhara, Mkataba wa Mtoto wa Afrika unatamka kuwa: “Ndoa za utotoni na kuchumbia watoto wa kike na wa kiume vitapigwa marufuku na hatua mathubuti, zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kutunga sheria ili umri wa chini wa ndoa kuwa miaka 18 na kufanya. uandikishaji rasmi wa ndoa uwe wa lazima”.
Majukumu ya dini na mila katika jamii za Kiafrika zinajulikana.
Ibara 1 kuhusu Wajibu wa Serikali Mwanachama wa Mkataba inasisitiza kuwa: “Kila desturi, mila, au taratibu za dini ambazo ziko kinyume na wajibu ulioko kwenye mkataba zisizingatiwe”.

## *Mikataba ya Kimataifa na Kisheria Juu ya ndoa za utotoni*

Mikataba mingi ya kimataifa imebainisha umuhimu wa umri wa chini wa kuingia kwenye ndoa na kusisitiza ulazima wa kuwa na ridhaa na uhuru katika ndoa kama namna ya kulinda haki za wanawake na watoto duniani kote. Kwa mfano, Azimio la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu linafafanua kuwa ndoa inatakiwa iwe ya hiari na wanandoa wawe watu wazima. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto unasisitiza kuwa umri wa chini wa ndoa ni miaka 18.

Mikataba ya Kisheria ya Kimataifa ina ufafanuzi zaidi ya umri na uhiari. Inaandaa mazingira ambayo inawalinda wanawake na wasichana na kuelekeza kuhusu kufurahia haki zao na misingi ya uhuru kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, na nafasi za kiraia na maeneo mengine. Kuridhia kwa Mikataba ya kisheria inaweza kusaidia kujenga fursa muhimu kwa ajili ya walio katika hatari ya kuingia kwenye ndoa za utotoni na wale walioolewa waweze kufikia malengo katika nyanja zote za maisha yao. Zaidi ya hayo, viwango ni kama vipimo vya uwajibikaji: serikali zinatakiwa kutoa taarifa kwenye kamati zinazofuatilia kuhusu utekelezaji.

Hata hivyo, kuridhia mikataba peke yake haitoshi; utekelezaji ni msingi. Katika mifumo kadhaa ya sheria kuridhia kwa mikataba, matokeo yake ya moja kwa moja ni matakwa ya mikataba hiyo kuingizwa kwenye sheria za nchi. Kwingine, mikataba ya kimataifa haina msukumo kisheria ndani ya nchi mpaka pale Sheria zitapotungwa kwa kufanya marekebisho ya kikatiba au kwa kupitisha sheria. Kwa kuongezea, nchi nyingi zina mfumo wa sheria nyingi ambapo sheria ya kawaida inatumika sambamba na sheria za dini na/au za kimila. Mara nyingi viwango vya kimataifa na vya kikanda na mara nyingine Katiba ya nchi haviendani na sheria za dini na kimila.

.

### Msimamo wa Nchi yako kuhusu Mikataba ya Kimataifa na Kisheria

| **Mkataba** *(*Pia ona Kiambatisho Na.1)* | **Imesainiwa** | **Imeridhiwa** | **Kipingamizi** | **Imetekelezwa** |
|---|---|---|---|---|
| Mkataba Nyongeza kuhusu kukomesha Utumwa, Biashara ya Utumwa na Taasisi na Taratibu zinazofanana na Utumwa. Ibara 1 (c) na 2 (1956) | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mkataba juu ya Ridhaa ya Ndoa, Umri wa chini wa Ndoa na Kuandikishwa kwa Ndoa Ibara 1, 2, na 3 (1964) | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake Ibara 2 na 16 (1979) | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za Kiuchmi, Kijamii na Kiutamaduni Ibara 10 (1976) | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |
| Mkataba wa Haki za Mtoto (1989) | ☐ | ☐ | ☐ | ☐ |

## *Vikwazo na Vizuizi katika kutekeleza sheria kuhusu ndoa za utotoni*

Vikwazo kadhaa vimejitokeza [18] na kama vikwazo hivyo viko nchini kwako, unalo jukumu la kutafuta ufumbuzi.

1. Kikwazo (K): Mfumo wa sheria unaogongana katika kuelekeza utaratibu wa ndoa na kufafanua mtoto ni nani.
   Ufumbuzi (U): *Fafanua mtoto ni nani kama ilivyo kwenye Mkataba wa Haki ya Mtoto, na umri wa chini wa kufunga ndoa utajwe kwa ajili ya wanaume na wanawake uwe miaka 18. Pitia mifumo ya sheria ili iwe na kiwango kimoja.*

2. (K): Ndoa nyingi zinafanyika nje ya mfumo rasmi wa sheria.
   (U): *Ongeza uelewa wa sheria kwa viongozi wa dini. na viongozi wa mila. Ingiza ulazima kwenye kutoa taarifa kuhusu ndoa za utotoni na utoe zawadi kwa kutoa taarifa.*
   .

3. (K): Vizazi na vifo haviandikishwi.
   (U): *Uandikishwaji wa vizazi na ndoa uwe ni lazima.*

4. (K): Uelewa potofu wa msimamo wa dini mbalimbali kuhusu umri wa kufunga ndoa.
   *(U): Kutana na viongozi wa dini ili kufanya mazungumzo. Kuza uelewa kuhusu namna mbadala za kutafsiri vitabu vya dini ili kukataa dhana kwamba ndoa za utotoni zinatakiwa na zimehalalishwa.*

5. (K): Ndoa za utotoni zimeenea zaidi vijijni ambako utekezezaji wa sheria una upungufu.
   *(U): Wawekwe Maafisa wa kuzuia ndoa za utotoni na kuwawezesha pamoja na kutoa mafunzo kwa wananchi wawe kama wasaidizi wa sheria.*

6. (K): Waathirika wa ndoa za utotoni chini ya sheria ni watoto. Hawana uwezo wa kufuatilia peke yao kesi mahakamani, kwa ujumla, tatizo ni kutokana na ukosefu wa rasilimali au ufahamu na maarifa kuhusu mifumo ya sheria.
   *(U): Kutoa taarifa juu ya matukio ihimizwe na ushauri wa kisheria utolewe kwa watoto bure.*

# 5 Majukumu ya Wabunge katika Kutokomeza ndoa za utotoni

Wabunge wana umuhimu mkubwa katika kutokomeza ndoa za utotoni kwa sababu, wanapitisha sheria, wanasimamia sera na kupitisha bajeti. Wabunge wenyewe wanalo jukumu kubwa katika kuweka suala la ndoa za utotoni katika agenda ya kisiasa na kuiagiza Serikali kupitisha mkabala utakaojumuisha mambo mengi na kuharakisha mabadiliko na kutokomeza tabia hiyo. Nafasi ya Wabunge ni ya kipekee kutokana na:

- kuwa mstari wa mbele katika kutunga sheria, kuhimiza maendeleo na kurekebisha sheria, na la muhimu zaidi ni utekelezaji wa sheria katika ngazi ya taifa.
  - Mazoea ya ndoa za utotoni inabidi yapigwe marufuku kisheria pamoja na sera ambazo zitatoa hatua za kuzuia na za kuleta nafuu kwa waathirika.
  - Utungaji wa sheria uwashirikishe jamii Asasi za Kiraia, viongozi wa kimila, na wa dini, makundi ya vijana, na wadau wanaohusika.
  - Sheria na sera kuhusu mimba za utotoni zinatakiwa ziwe sehemu ya mfumo mpana unaolenga kuhakikisha wasichana na wanawake wanafurahia na kutekelezewa haki zao.
  - Sheria inabidi iende sambamba na mafunzo mathubuti katika mahakama na taasisi nyingine zenye wajibu wa kutekeleza sheria.
- Kuhakikisha kuoanisha mikataba ya kimataifa na kama inavyofaa pamoja na mikataba ya kikanda na sheria za nchi. Kuhakikisha utekezaji wa mikataba na sheria na kusambaza maudhui ya sheria kwa wananchi na mahakama.
- Hakikisha kuwa serikali inatengeneza Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza ndoa za utotoni na kuzindua kampeni za kuongeza uelewa au juhudi nyingine zenye mtazamo wa muda mrefu wa kukomesha ndoa za utotoni.
- Fafanua mipangilio ya bajeti inayohitajika ili kuhamasisha rasilimali za kitaifa kwa ajili za juhudi za kifedha ili kutokomeza ndoa za utotoni, ikiwa ni pamoja na, lakini siyo tu wizara, mipango kazi na kampeni za kitaifa, huduma za kijamii n.k.
- Kusimamia utekelezaji wa sera na sheria na kudai uwajibikaji kutoka taasisi na watendaji wanaohusika na kukomesha mimba za utotoni na kuwalinda wasichana dhidi ya hatari pamoja na walioolewa.
- Kuhakikisha kutokomeza mimba za utotoni inaimarisha utungaji wa sera na kutekeleza mikakati katika wizara zinazohusika.
- Kujenga ushirikiano mpya, kutengeneza mazingira kwa ajili Asasi za Kiraia kushirikiana na serikali ili kuhakikisha mkabala unaojumuisha mambo mbalimbali ya kushughulikia ndoa za utotoni.
- Kuwakilisha matatizo ya maeneo mbalimbali pamoja na, kuzungumzia mahitaji ya wanawake na wasichana.

## Nchi yako inasimamia wapi juu ya Sheria na Sera ngazi ya taifa?

| Sheria na sera | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|
| Nchi yako imeweka utaratibu wa umri wa chini wa ndoa kwa vijana wa umri wa miaka 18? | ☐ | ☐ |
| Je! Sheria inakataza ndoa za utotoni? | ☐ | ☐ |
| Je! sheria zinahitaji hiari na mapatano kamili kwa ajili ya ndoa kwa pande zote mbili za mwanamume na mwanamke? | ☐ | ☐ |
| Ruhusa ya wazazi au vipingamizi vingine vinaweza kutumiwa kumlazimisha msichana? | ☐ | ☐ |
| Nchi yako ina mfumo wenye ufanisi wa uandikishaji wa vizazi na ndoa? | ☐ | ☐ |
| Je! watekelezaji wa sheria wanatekeleza sheria kwa ufanisi na kutekeleza mfumo wa sheria kwa ajili ya kuzuia mimba za utotoni na kuwalinda watoto wa kike walioolewa.? | ☐ | ☐ |
| Nchi yako ina sheria zinazohakikisha usawa wa kijinsia katika ndoa na inapovunjika? | ☐ | ☐ |
| Je! Nchi yako ina Mpango Kazi wa kitaifa kwa ajili ya kutokomeza ndoa za utotoni? | ☐ | ☐ |
| Kuna mifumo ya sera ya kutosha pamoja na vyanzo vya rasilimali kwa ajili kutoa msaada kwa watoto wa kike walio katika hatari ya kuolewa na walioolewa.? | ☐ | ☐ |

# 6 Wabunge wanaweza kufanya nini?

### *Chukua hatua*

- Panga mikutano isiyo rasmi na wabunge wenye msimamo wa kutokomeza ndoa za utotoni ikifuatiwa na kuwasilisha, kwenye kamati za bunge zinazohusika kwa nia ya kuongeza uelewa wa Wabunge kuhusu hali ya ndoa za utotoni nchini na haja ya kushughulikia suala hilo kwa namna ambayo inajumuisha mambo mbali mbali.
- Kuanzisha jukwaa la Wabunge dhidi ya ndoa za utotoni.
- Kushiriki kikamilifu katika majadiliano juu ya mgao wa bajeti kwa ajili ya kuzuia ndoa za utotoni, sera na programu za kukabiliana na tatizo hilo. Pia kutoa msaada kwa ajili, ya mgao wa bajeti kwa ajili ya sera na programu ambazo zitajenga mazingira ya wasichana kuweza kufikia uwezo wao kamili kama vile elimu, programu za kijamii ' na kiuchumi kwa wasichana walioacha shule, mipango ya ulinzi wa watoto na wanawake, malazi, ushauri nasaha wa kisheria, na ushauri nasaha wa kisaikolojia, n.k.
- Kukutana na Asasi za Kiraia na watendaji wengine wanaofanya kazi ya kutokomeza ndoa za utotoni katika jimbo lako. Kupitia miradi ili kujifunza kuhusu mbinu zinazotumika. Kuzungumza na wasichana, wazazi na viongozi wa kijamii ili kujifunza kuhusu shida zao.
- Kukuza mazungumzo na viongozi wa serikali za mitaa katika jimbo lako ili kuwaelewa watendaji na mawazo yao juu ya ndoa za utotoni.
- Kujenga uwezo wako na maarifa kuhusu ndoa za utotoni ili kuwa wakala wa mabadiliko katika jimbo lako na katika nchi yako.
- Kuwa sauti imara katika kujenga uelewa wa umma juu ya ndoa za utotoni, zilivyoenea, watendaji ni kina nani na madhara yake na kutoa rai kwa uongozi wa serikali na kuwekeza katika kuzuia na namna ya kukabiliana na tatizo.

### *Uwajibike na udai uwajibikaji*

- Kutoa mrejesho wa uzoefu kwa Wabunge wengine na kamati za bunge zinazohusika, kwa mfano, kufanya vikao baada ya kuhudhuria mkutano, mafunzo, kufanya ziara, au matukio mengine kuhusu ndoa za utotoni.
- Kushikamana na kutoa taarifa kwa asasi za kiraia zinazoshughulikia ndoa za utotoni au maendeleo yoyote ya kibunge. Unaweza kujitolea kuandaa mikutano, majadiliano ya meza na mazungumzo ya kawaida n.k.
- Fanya usikilizaji wa hadharani kila mwaka kuhusu ufuatiliaji na utekelezaji wa sheria.
- Dai uwajibikaji kutoka kwa mawaziri na wadau wengine. Wahoji hao wenye wajibu wa kutokomeza ndoa za utotoni, fuatilia hali ya ndoa za utotoni nchini na matokeo yake.
- Dai uwajibikaji na utoaji wa taarifa za Mikataba ya Kimataifa na Kikanda zilizoandaliwa kwa wakati na kwa kina kwa mfano Mkataba wa Kimataifa wa kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake.

## Ikuze nchi yako kama bingwa wa kimataifa dhidi ya ndoa za utotoni

### *Kushirikisha mazungumzo – kipindi cha baada ya 2015 cha mfumo wa maendeleo*

Mfumo wa maendeleo wa baada ya 2015 ambao ni mrithi Malengo ya Milenia utaweka msingi wa maendeleo kitaifa na kimataifa kuhusu vipaumbele vya maendeleo katika miaka 15 ijayo.

Wakati ndoa za utotoni moja kwa moja ni kikwazo katika kufikia malengo namba 6 na 8 katika Malengo ya Milenia, wasichana wadogo walisahaulika katika malengo hayo. Hivi sasa haki na mahitaji ya watoto wa kike vinatambulika kuwa lazima viwe ni msingi katika mfumo wa maendeleo.

Malengo ya Maendeleo Endelevu baada ya mwaka 2015 yataruhusu kuhusisha kazi za serikali kitaifa na mipango mikubwa ya kimataifa. Kwa Wabunge kujihusisha na Mfumo wa Maendeleo baada ya 2015 katika kazi zao wataweza kutoa huduma, kwenye majimbo yao na kuleta mabadiliko mapana ya kijamii na uchumi.

- Hamasisha serikali yako itoe msaada wenye lengo la kutokomeza ndoa za utotoni katika Mfumo wa Maendeleo baada ya 2015. Kuenea kwa ndoa za utotoni ni kiashiria kinachopimika na kilichofafanuliwa chenye vipaumbele vya maendeleo mbalimbali na vinaweza kufuatiliwa kwa ukakika kwa muda katika nchi nyingi. Tayari ufuatiliaji maalum umefuatia kwa kutumia tafiti za kitaifa zinazofanyika mara kwa mara kwa kupishana.
- Mhamasishe kiongozi wa nchi yako au mawaziri wahusika kuzungumza mbele ya Baraza la Umoja wa Mataifa au kwenye tukio jingine kuhusu umuhimu wa kulenga kushughulikia ndoa za utotoni katika Mfumo wa Maendeleo baada ya 2015.
- Mkaribishe Waziri wa Mambo ya Nje na Mawaziri kadhaa kwa kuwapa ufafanuzi kuhusu vipaumbele vyao katika mfumo wa maendeleo baada ya 2015 na kusisitiza kuhusu umuhimu wa kuweka lengo la kutokomeza ndoa za utotoni katika dhamira ya usawa wa kijinsia na kuwawezesha wasichana na wanawake.
- Toa hoja bungeni kwa ajili ya wizara husika ili watoe ufafanuzi kuhusu kuhusika kwao na vipaumbele katika mazungumzo kuhusu Maendeleo Endelevu baada ya 2015 yatakayoanza Januari 2016. Sisitiza kuwa ndoa za utotoni lazima zishughulikiwe kimkakati na kwa ukamilifu katika mfumo wa maendeleo baada ya 2015.
- Wasilisha taarifa bungeni ili maamuzi yatolewe juu ya Maendeleo Endelevu baada ya -2015 na ndani ya Mfumo wa Bunge au taasisi nyingine za Kibunge kwenye kanda.
- Andaa tukio au mkutano wa hadhara kuhusu mimba za utotoni ndani ya Bunge na tafuta uwezekano wa kuwakaribisha wataalam husika kutoka Umoja wa Mataifa na wawakilishi wa asasi za kiraia na ikiwezekana, watafiti, wanataaluma, waandishi wa habari n.k.
- Toa ushauri kwamba wawakilishi wa Wabunge wawe kwenye Misafara ya Kiserikali kwa ajili ya mazungumzo ya Mfumo wa Maendeleo baada ya 2015.

### Kujihusisha na Umoja wa Mataifa Baraza la Haki za Binadamu

- Hakikisha Makubaliano katika taarifa za Mikataba ya Haki ya Mtoto na wa Ubaguzi dhidi ya Wanawake ni pamoja na:
  - Taarifa za vipindi kujumuisha ripoti kuhusu ndoa za utotoni.
  - Bunge kuhusika katika maandalizi ya ripoti kwa kutoa taarifa juu ya ndoa za utotoni au kwa kupewa taarifa ya kilichomo kwenye ripoti hizo.
  - Bunge kuwasilishiwa na kupata fursa ya kujadili chunguzi za kamati za Umoja wa Mataifa.
- Tafuta kujua kama nchi yako ni sehemu ya kundi la msingi linalolifanyia kazi Azimio la Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2015. Kama siyo, ishawishi nchi yako ijiunge na kundi na kuunga mkono azimio mathubuti na lenye kina juu ya ndoa za utotoni.

### Wafikie wengine na ushirikiane

- Fanya kazi na Wizara husika, hamasisha ushirikiano katika mambo mbali mbali katika ngazi, za kikanda na kimataifa.
- Shiriki kikamilifu katika mitandao ya Wabunge katika kanda yako na kimataifa, ili kubadilishana uzoefu wa kushughulikia ndoa za utotoni, na kuendeleza utashi wa kisiasa.
- Unga mkono kampeni za kitaifa, kikanda na kimataifa ili kutokomeza ndoa za utotoni, kwa mfano, kushiriki, mikutano na matukio, kutoa hotuba, kwa kuhojiwa na kadhalika.
- Wakaribishe wataalamu wa ndoa za utotoni na wawakilishi wa asasi za kiraia kuwa wazungumzaji rasmi katika Mikutano ya nje ya Wabunge na katika fursa nyingine za kuongeza uelewa.

### Jenga Kujulikana na Ongeza Uelewa

- Tumia Mitandao ya kiasili na ile ya kijamii (blogs, Twitter, Facebook, Op-eds, machapisho n.k,) kulijulisha jimbo kuhusu ndoa za utotoni na juhudi za serikali katika kulishughulikia.
- Andika tamko kwa ajili ya Vyombo vya Habari na andaa mkutano kwa ajili ya wanahabari – k.m. baada ya kuhudhuria mkutano, kushiriki mazungumzo katika ngazi za juu n.k.
- Tumia sherehe za siku maalum za kimataifa kwa ajili ya kuongeza uelewa juu ya ndoa za utotoni (kwa mfano, Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike – 11 Oktoba).
- Hamasisha vyombo vya habari vihusike na midahalo, kutoa taarifa na kuongeza uelewa juu ya ndoa za utotoni.

# 7 viambatisho

## i. Ibara katika mikataba ya kimataifa inayohusika na ndoa za utotoni

**Azimio la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu (1948)**

**Ibara ya 16:**

(1) Watu wazima waume kwa wake, bila kizuio chochote kwa sababu ya rangi, taifa, au dini wana haki sawa ya ndoa na kuwa na familia. Wanayo haki sawa ya ndoa, wakati wa maisha yao ya ndoa na wakati wa kutenguka ndoa.

(2) Ndoa inaweza kufungwa tu kwa hiari na mapatano kamili kati ya hao wanaotaka kuoana.

(3) Familia ni kiungo cha asili cha jamii ya watu, na inastahili kulindwa na watu pamoja na serikali.

.

**Mkataba wa Ziada wa Kukomesha Utumwa, Biashara ya utumwa na Taasisi na Desturi sawa na Utumwa (1956)**

**Ibara 1** : Kila serikali mwanachama wa Mkataba huu itachukua hatua muhimu zinazotekelezeka za kisheria na hatua nyinginezo ili hatua kwa hatua na bila kuchelewa iweze kufuta au kuziacha taasisi na desturi zifuatazo ambazo bado zipo na zile zilizoainishwa au vinginevyo kwenye ufafanuzi wa utumwa katika ibara ya 1 ya Mkataba wa Utumwa uliotiwa saini Geneva Septemba 1926.

(c) Taasisi yoyote au desturi ambapo:

(i) Mwanamke bila haki ya kukataa, anaahidiwa ndoa, au anaozwa kwa malipo ya fedha au kwa mali wanayopewa wazazi, mlezi, familia au mtu mwingine au kikundi; au

(ii) Mume wa mwanamke, familia yake au ukoo wake, wana haki ya kumhamisha kwenda kwa mtu mwingine kwa thamani iliyopokelewa au vinginevyo; au

(iii) Mwanamke anapofiwa na mumuwe anawajibika kurithiwa na mtu mwingine.

**Ibara 2** : Kwa ajili ya kufuta taasisi na desturi zilizotajwa katika Ibara 1(c) ya Mkataba huu, nchi wanachama wa Mkataba huu zitaweka viwango pale inapofaa, umri wa chini unaofaa kwa ajili ya ndoa, kuhamasisha utumiaji wa nafasi zilizopo ambapo makubaliano ya wanandoa yanaweza kutolewa kwa uhuru mbele ya mamlaka husika za kiraia au kidini, na kuhamasisha uandikishaji wa ndoa.

.

**Mkataba wa Kimataifa wa Makubaliano ya Ndoa, Umri wa Chini wa Ndoa na Kuandikishwa kwa Ndoa (1964)**

**Ibara 1**

1. Hakuna ndoa itakayofungwa kisheria bila makubaliano kamili na huru kutoka kwa wanandoa, makubaliano hayo yatolewe na wanandoa wenyewe baada ya kutangazwa mbele ya mamlaka husika ya kufungisha ndoa na ni pamoja na kuwepo mashahidi kama inavyoelezwa kisheria.
2. Pamoja na kitu chochote kilichopo kwenye aya 1 hapo juu, haitakuwa lazima kwa mwanandoa mmoja wapo kuwepo wakati mamlaka husika imeridhika kuwa hali ni ya kipekee, na kwamba mwanandoa asiyekuwepo mbele ya mamlaka husika na kwa namna inayokubalika kisheria ametamka na amekubali.

.

**Ibara 2** : Nchi mwanachama wa Mkataba huu itatunga sheria inayotamka umri wa chini wa kuingia kwenye ndoa. Hakuna ndoa kisheria kwa mtu yoyote chini ya umri huo isipokuwa pale ambapo mamlaka husika imetoa ruhusa kuhusu umri kutokana na sababu nzito kwa maslahi ya wanandoa watarajiwa.

.

**Ibara 3** : Ndoa zote zitaandikishwa rasmi kwa utaratibu unaohifadhiwa na mamlaka husika.

## Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Raia na Siasa, 1966

**Ibara 23(2)** : Haki ya wanaume na wanawake wa umri wa kuolewa/kuoa na kuanzisha familia itatambuliwa.

**Ibara 23(3)** : Hakuna ndoa inayoweza kufungwa bila hiari na mapatano kamili kati ya hao wanaotaka kuoana.

**Ibara 23(4)** : Mataifa wanachama wa Mkataba huu watachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha usawa wa haki na wajibu wa mume na mke wakati wa ndoa na wakati wa ndoa kuvunjika.

## Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (1976)

**Ibara 10** : Nchi wanachama wa Mkataba huu wanatambua kwamba:

1. Ulinzi mpana iwezekanavyo na msaada lazima vipewe familia, ambayo ni kiungo asili na cha msingi katika jamii, hasa kwa kuanzishwa kwake na huku ikiwa na jukumu la kutunza na kuelimisha watoto wanaoitegemea. Ni lazima ndoa iwe ya wanandoa watarajiwa waliokubaliana kwa uhuru.

## Mkataba wa Kimatifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979)

**Ibara 2** : Nchi wanachama zinalaani ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya wanawake, zinatafuta namna inazofaa na bila kuchelewa kutunga sera ya kutokomeza ubaguzi dhidi ya wanawake na kufanya yafuatayo:

**Ibara 16**

(1): Nchi wanachama watachukua hatua muhimu zinazotakiwa kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake katika mambo yote yanayohusu ndoa na mahusiano ya kifamilia na hasa itahakikisha kutokana na misingi ya usawa kati ya wanaume na wanawake.

(a) Haki sawa ya kuingia kwenye ndoa;

(b) Haki sawa ya kuchagua mwenzi wa ndoa na kufunga ndoa kwa makubaliano kamili yaliyo huru na kwa hiari;

(2): Uchumba na ndoa ya mtoto haina uhalali kisheria na hatua zote na muhimu ikiwa ni pamoja na, hatua za kisheria, zitachukuliwa kutamka umri wa chini wa kuoa na kuolewa na kuweka ulazima kwenye kuandikisha ndoa rasmi.

## Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto (1989)

**Ibara 1**: Mtoto ni mtu yoyote chini ya miaka 18 isipokuwa pale ambapo chini ya sheria husika ya mtoto, umri wa mtu mzima umefikiwa.

**Ibara 2**: Uhuru wa kutokubaguliwa kwa sababu yoyote, pamoja na kutokuwepo ubaguzi wa kijinsia, dini, kabila, au asili ya kijamii, kuzaliwa au hali nyingine.

**Ibara 3**: Kimsingi hatua zote kuhusu watoto… maslahi bora ya mtoto yatakuwa msingi wa kuzingatiwa.

**Ibara 6**: Juhudi kubwa kuhusu kuishi kwa mtoto na maendeleo yale.

**Ibara 12**: Haki ya mtoto ya kutoa mawazo yake kwa uhuru katika mambo yote yanayomgusa mtoto kulingana na umri na anavyokua kuelekea kuwa mtu mzima.

**Ibara19**: Haki ya kulindwa kutokana na aina zote za ukatili wa kimwili au kiakili, kuumia au dhuluma, uonevu au unyonyaji, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, wakati wa kuhudumiwa na wazazi, walezi au mtu mwingine yoyote.

**Ibara 24**: Haki ya afya na ya upatikanaji wa huduma za afya; na kulindwa kutokana na madhara ya taratibu za tamaduni.

**Ibara 28 and 29**: Haki ya kupata elimu kwa misingi ya fursa sawa.

**Ibara 34**: Haki ya kulindwa kutokana na aina zote za unyonyaji, kingono na unyanyasaji wa kijinsia.

**Ibara 35**: Haki ya kulindwa kutokana na utekaji, uuzaji au usafirishaji wa binadamu

**Ibara 36**: Haki ya kulindwa kutokana na aina zote za unyonyaji ambao una madhara kwa kipengele chochote cha ustawi wa mtoto.

## Sampuli ya maswali ya kuwauliza mawaziri na wengine muhimu wanaofanya maamuzi

### Hoja kwa serikali kutoa taarifa juu ya hali ya ndoa za utotoni katika nchi yako kwa kujibu maswali yafuatayo:

- Kitaifa kiwango cha ndoa za utotoni kiko je?
- Je! wasichana katika mikoa gani hasa wako katika hatari zaidi ya ndoa za utotoni?
- Viwango vya kitaifa vinalinganishwa je na nchi nyingine katika kanda?

### Hoja kwa Waziri wa Elimu kutoa majibu kwa maswali yafuatayo:

- Kiwango gani cha wasichana wanaoingia shule za msingi na sekondari, pamoja na fursa za elimu isiyo rasmi?
- Unahakikishaje utoaji wa elimu unashughulikia mambo yanayoathiri kujiamini au uwezo wa familia wa kuwaweka watoto shuleni, kama vile, wasiwasi kuhusu kusafiri au kutembea kwenda shuleni, usalama shuleni, usafi wa mazingira na ukatili wa kijinsia?
- Unahakikisha je watoto wa kike na wasichana walioolewa kisheria au kiuhalisia hawakoseshwi elimu yenye viwango?
- Unashughulikia je vikwazo vya kifedha kwa ajili ya wasichana ili waendelee na elimu?
- Unasaidia je katika mipango ya kina ya elimu ya uzazi katika programu shuleni, katika jamii; kusaidia kuhoji na kubadilisha hali ya kutokuwepo usawa wa kijinsia, kanuni katika jamii na ubaguzi na kuwawezesha wasichana kuielewa miili yao na haki zao?
- Je! Walimu na watu wengine wenye mamlaka wamepewa mafunzo ili waweze kutambua namna ya kushughulikia na kutoa taarifa kuhusu mimba za utotoni?

### Hoja kwa Waziri wa Sheria kutoa majibu kwa maswali yafuatayo:

- Unahakikisha mamlaka za utekelezaji wa sheria zinatumia sheria zilizopo juu ya ndoa za utotoni?
- Watekelezaji wa sheria wamepata mafunzo ya aina gani kuhusu ndoa za utotoni?
- Namna gani unahuisha sheria za kimila na sheria za nchi ili kukwepa mianya ya kutokwenda sambamba?
- Ni kesi ngapi za ndoa za utotoni zimeripotiwa katika mwaka uliopita?

### Hoja kwa Waziri wa Afya ajibu maswali yafuatayo:

- Kuna huduma gani kwa watoto wa kike walioolewa? Hizo huduma zinawafikia watoto hao wa kike?
- Kuna kiwango gani cha uelewa kuhusu madhara ya kiafya ya ndoa za utotoni katika jamii na watumishi wa afya?
- Ni kiwango gani cha kitaifa cha watoto wa kike wanaopata mimba?
- Huduma gani zinapatikana za afya ya kujamiana na ya uzazi kwa ajili ya wasichana?
- Ni jinsi gani utasaidia programu ya kina ya elimu ya ngono katika shule na jamii, ili kusaidia kuhoji na kubadilisha kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia, kanuni na mazoea yenye ubaguzi na kuwawezesha wasichana kuielewa miili yao na haki zao?

## iii. Sampuli ya ujumbe katika mitandao ya kijamii

**Kukomesha ndoa za utotoni ni muhimu:**

- Kimataifa wanawake 720 walio hai leo waliolewa kabla ya kufikia miaka 18, au takriban 10% ya watu duninani. Hatuwezi kudharau. #komesha ndoa za utotoni
- Wasichana hai 280 milioni leo wako katika hatari ya ndoa za utotoni kwa mujibu wa Shirika la, Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF) na @GirlsNotBrides http://bit.ly/1lEGDKZ
- Nchi zitaendelea je kama ½ ya watu wake wanaachwa nyuma? #kukomesha ndoa za utotoni ni ufunguo wa maisha bora ya baadaye na yanazingatia usawa http://bit.ly/1ijkERO
- #ndoa za utotoni siyo suala liliojitenga na kusimama peke yake. Linaathiri juhudi zetu za kukomesha umaskini, ukatili & namna ya kuboresha afya, elimu kwa wote. #post2015

**Ni nini matokeo ya ndoa za utotoni?**

- Hii inaonesha maana ya ndoa za utotoni kwa mamilioni ya wasichana walioolewa kabla ya kufikia miaka 18: http://bit.ly/ZnPff0
  Tufanye kazi pamoja kutokomeza ndoa za utotoni!
- # Ndoa za utotoni ni mitego kwa wasichana, familia zao & jamii katika mzunguko wa umaskini baina ya vizazi http://bit.ly/14dPn0U #post2015
- Mara nyingi, #ndoa za utotoni ni alama ya wasichana kukosa elimu http://bit.ly/1hpBWMW #komesha ndoa za utotoni #post2015
- Watoto wa kike wanaozaa kabla ya kufikia miaka 15 wana uwezekano wa mara 5 zaidi wa kufariki wakati wa kujifungua kuliko wanawake katika miaka ya mwanzo ya 20. http://bit.ly/1wFu5Ev #post2015
- Wasichana wanaoolewa kabla ya miaka 18 wako kwenye uwezekano wa kufanyiwa ukatili katika ndoa kuliko wasichana wanaoolewa baadaye. http://bit.ly/1bkss7x #post2015
- # ndoa za utotoni zimepunguza kasi ya maendeleo ya malengo namba 6 kati ya 8 ya Malengo ya Millennia (MyM). Wakati umefika wa kushughukia suala hili katika mfumo wa maendeleo wa baada ya mwaka 2015. @GirlsNotBrides

**Kwa nini ndoa za utotoni zinatokea?**

- Sababu za msingi za kuwepo kwa ndoa za utotoni ni ngumu: umaskini, mila, na kutokuwepo usawa wa jinsia, mara nyingi zinaongezeka kunapokuwepo na migogoro. http://bit.ly/15dT54Y
- #Ndoa za utotoni zimekuwepo katika baadhi ya jamii kwa vizazi, lakini mila potofu zinaweza kubadilika. http://bit.ly/15dT54Y

**Ni nini kinatakiwa ili kukomesha ndoa za utotoni?**

- Kutokomeza ndoa za utotoni lazima ziwe ni lengo maalum katika mfumo wa maendeleo ya baada ya mwaka 2015, kama tuna nia ya kuweko kwa maendeleo katika elimu, afya ya uzazi au kuondoa umaskini.
- Sheria hazitoshi kukomesha ndoa za utotoni. Tunahitaji tuwekeze kwenye sera, huduma & programu zenye njia mbadala kwa wasichana.
- Tunafahamu ni nini kinafanya kazi ili kutokomeza ndoa za utotoni. Sasa tunatakiwa tuwekeze kwenye programu & kuziongeza kwa ajili ya matokeo yenye upeo. http://bit.ly/1gb3fv2
- Uratibu & hatua za kina kati ya afya, haki, elimu & sekta ya fedha ambazo ni misingi katika kukomesha ndoa za utotoni: http://bit.ly/1rfBU4j

## iv. Nyenzo za kupakua kutoka mitandaoni

**Kwa ufupi:**

- Uelewa wa ukubwa wa tatizo la ndoa za utotoni – inatoa takwimu mbalimbali ili kujadili ukubwa wa tatizo na kulinganisha kwa namna ambako kunafanya takwimu ziwe na maana kwa watu wengi zaidi.
- Nadharia ya mabadiliko kuhusu ndoa za utotoni – kielelezo cha kuchora kinachoonyesha aina mbambali za mitezamo inayohitajika kushughulikia ndoa za utotoni na namna zinavyoshabihiana. Ikiungwa mkono na historia fupi na mwongozo kwa mtumiaji.

**Vifaa vinavyoleta sauti na picha (video):**

- *“Together: Ending child marriage in Zambia”*– Sinema hii ni hadithi ya namna wanaharakati wa asasi za kiraia, wasichana, viongozi wa mila na serikali wanavyoweza kushirikiana huko Zambia ili kuhakikisha hakuna msichana anayeolewa akiwa mtoto.
- *“The world we want: End child marriage"*– Sinema hii inafafanua namna tunavyoweza kufanya kazi pamoja ili kufanya ndoa za utotoni ziwe historia na kuboresha maisha ya mamilioni ya wasichana kote duniani.
- *“Traditions can change: Ending child marriage”*– katika *“video”,* hii Graça Machel, Mary Robinson and Desmond Tutu kati ya kundi la watu wazima wanatoa rai kwa watu duniani kote kuchukua hatua: ya kutokomeza ndoa za utotoni katika kizazi kimoja.

**Maelezo ya michozo:**

Bofia ili utezame kutoka kwenye mtandao/kupakua.













Kwa ajili ya taarifa na machapisho juu ya ndoa za utotoni tezama:

www.girlsnotbrides.org/reports-and-publications/

## v. Machapisho kuhusu ndoa za utotoni na sheria


- Center of Reproductive Rights, *Child Marriage in South Asia: International and Constitutional Legal Standards and Jurisprudence for Promoting Accountability and Change*, 2013. http://www.girlsnotbrides.org/reports-and-publications/child-marriage-in-south-asia-international-and-constitutional-legal-standards-and-jurisprudence-for-promoting-accountability-and-change/

- Equality Now, *Protecting the girl child: Using the law to end child, early and forced marriage and related human rights violations*, 2014. http://www.girlsnotbrides.org/wp-content/uploads/2014/01/Equality-Now-Protecting-the-Girl-Child-JAN-2014.pdf
- Ford Foundation, *Ending Early Marriage Through Legal, Rights Based and Public Policy Approaches*, 2013.
- OHCHR, *Preventing and eliminating child, early and forced marriage*, 2014. http://www.girlsnotbrides.org/new-ohchr-report-child-early-forced-marriage/
  - UNICEF, *Child Marriage and the Law*, 2007. http://www.unicef.org/french/files/Child_Marriage_and_the_Law.pdf


### vi. Maelezo ya jumla na takwimu:


- UNFPA, *Marrying too Young: End Child Marriage*, 2013. http://www.unfpa.org/webdav/site/global/shared/documents/publications/2012/MarryingTooYoung.pdf
- UNICEF, *Ending Child Marriage: Progress and Prospects*. 2014 http://data.unicef.org/corecode/uploads/document6/uploaded_pdfs/corecode/Child-Marriage-Brochure-7_17-HR_164.pdf


## vii. Vifupisho

MKHKK – Mkataba wa Kimataifa wa Kukomeza Haki za Kiraia na Kisiasa
MKHKKU – Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, Kiuchumi na Utamaduni
MKHM – Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto
MKKUDW – Mkataba wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake
MyM – Malengo ya Milenia
UNFPA – *United Nations Population Fund*
UNICEF - *United Nations Children's Fund*

## viii. Maelezo ya mwisho


1. Mikakati mingine ni: Kuwawezesha Wasichana, Uhamasishaji wa Familia na Jamii, na Utoaji wa Huduma http://www.girlsnotbrides.org/reports-and-publications/theory-change-child-marriage/
2. Rangita de Silva de Alwis, *Child marriage and the law, Legislative Reform Initiative Paper Series*, UNICEF, 2008 (p. 37)
3. UNICEF, *Ending Child Marriage: Progress and prospects*, 2014
4. UNICEF, *The State of the World's Children*, 2014
5. *Idem*.
6. Kulingana na uchambuzi wa taarifa za Utafiti wa Watu na Afya (DHS) na Utafiti wa Viashiria mbalilmbali katika nguzo za maendeleo (MICS), *kwa nchi 48, 1986-2006 na 2001-2010, UNFPA, Marrying too Young: End Child Marriage, 2012.*
7. UNICEF, *The State of the World's Children, Adolescence: An Age of Opportunity*, 2011
8. International Center for Research on Women, *How to End Child Marriage: Action Strategies for Prevention and Protection*, 2007
9. International Center for Research on Women, *Child Marriage Factsheets: Child Marriage and Poverty*, 2007
10. IPPF and the Forum on Marriage and the Rights of Women and Girls, *Ending child marriage: a guide for global policy action*, 2006; International Center for Research on Women, *Too Young to Wed: Education & Action towards Ending Child Marriage: Seeking Policy Solutions*, 2005
11. UNICEF, *Early Marriage: Child Spouses*, UNICEF Innocenti Research Centre, 2001
12. Kishor, S. & Johnson, K., *Profiling Domestic Violence – A Multi-Country Study*, ORC Macro, Calverton, Maryland, 2004
13. IPPF and the Forum on Marriage and the Rights of Women and Girls, *Ending child marriage: a guide for global policy action*, 2006
14. Levine, R., Lloyd, C., Greene, M., & Grown, C., *Girls Count: A Global Investment and Action Agenda*, Center for Global Development, 2008
15. UNFPA, *Motherhood in Childhood, Facing the Challenge of Adolescent Pregnancy*, 2013
16. UNFPA, *State of World Population*, 2005
17. WHO, *Guidelines on preventing early pregnancy and poor reproductive outcomes in adolescents in developing countries*, 2011
18. Ford Foundation, *Ending Early Marriage Through Legal, Rights-Based and Public Policy Approaches in West Africa*, 2013




Design: Ben Cave

*Watoto wa Kike siyo Mabibi harusii*

Ni ushirikiano wa kimataifa wa asasi za kiraia zadi ya 400 katika nchi zaidi ya 60 zenye dhamira ya kutokomeza ndoa za utotoni na kuwawezesha wasichana kufikia uwezo wao.

*Girls not Brides: Global Partnership to End Chid Marriage*
Brook Green, First Floor, Building 5
50 Brook Green
London W6 7BJ
United Kingdom

Registered Charity No: 1154230

Cover rah rou iri ot rid

Za kiraia zadi ya 400 katika nchi zaidi ya 60
zenye dhamira ya kutokomeza mimba za utotoni
kufikia uwezo wao

*Watoto wa kike siyo mabibi harusi:* Ushirikiano wa kimataifa *kutokomeza ndoa za utotonii*
Brook Green, First Floor, Building 5
50 Brook Green
London W6 7BJ
United Kingdom

Registered Charity No: 1154230

Cover rah rou iri ot rid

www.GirlsNotBrides.org